








Watoto wa nta

-  Southern African Folktale
-  Wiehan de Jager
-  Mutugi Kamundi
-  Kiswahili
-  Level 2







Hapo zamani za kale, paliishi familia yenye furaha.




Hawakugombana hata kidogo. Watoto waliwasaidia wazazi nyumbani na shambani.




Lakini, walikatazwa kwenda karibu na moto.




Walifanya kazi zao zote usiku. Hii ni kwa sababu walikuwa wameumbwa kwa nta.




Lakini, kijana mmoja alitamani kwenda nje wakati wa mchana.




Siku moja tamaa ya kwenda nje ikazidi. Wenzake wakamwonya asiende juani. Lakini, hakisikia.




Aliyeyuka kwa sababu joto lilikuwa kali.




Watoto wa nta walihuzunika walipoona kaka yao
akiyeyuka.



Wakapanga jambo fulani. Walichukua nta iliyoyeyuka wakatengeza ndege.



Wakamweka ndege huyo juu ya mlima mrefu.



Jua lilipochomoza asubuhi, akapeperuka akiimba kwa furaha.



Storybooks Outline

global-asp.github.io/storybooks-outline

Watoto wa nta

Written by: Southern African Folktale

Illustrated by: Wiehan de Jager

Translated by: Mutugi Kamundi

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by [Storybooks Outline](#) in an effort to provide children's stories in the world's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).